

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**Halmashauri ya Manispaa ya Lindi.**

Telegraphic address  
Tel: 023-220-2164  
Fax: 023-220-2116  
E-mail: info@lindimc.go.tz



Mkurugenzi wa Manispaa  
S.L.P 1070,  
LINDI.

Barua zote zielekezwe kwa Mkurugenzi wa Manispaa

**Kumb Na: LMC/D.10/6/31**

**7 Agosti, 2019.**

Mkurugenzi Mkuu,  
ACSHO Company Ltd,  
S.L.P 14190  
**DAR ES SALAAM.**

**YAH: KURIDHIA OMBI LA EKARI 500 KWA AJILI YA UWEKEZAJI.**

Rejea mada tajwa hapo juu pamoja na barua yako ya tarehe 24 Julai, 2019 uliyoiandikia ofisi ya Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Lindi. Katika barua ile uliomba kupatiwa Ardhi yenye ukubwa ekari 500 kwa ajili ya kilimo cha Ufuta.

Itakumbukwa kuwa mnamo mwezi Machi 2019, Mkoa wa Lindi kwa kushirikiana na kampuni ya magazeti ya Serikali "Tanzania Standard Newspapers" (TSN) uliandaa na kuendesha kongamano la fursa za uwekezaji. Kupitia kongamano hilo, Halmashauri ya Manispaa ya Lindi ilitoa mwaliko wa uwekezaji katika sekta mbalimbali ikiwemo Kilimo ambapo mazao ya Ufuta, Alizeti na Korosho yalielezwa kuwa ni ya kimkakati.

Kwa barua hii, ninayo furaha kukutaarifu kuwa maombi yako ya kupatiwa ekari 500 kwa ajili ya kilimo cha Ufuta na mazao mengine ya mbegu za mafuta hususani Alizeti yamekubaliwa rasmi. Hivyo, kampuni yako inaelekezwa kuchangia kiasi cha Tsh 100,000.00 kwa kila ekari moja ili iweze kupatiwa Ardhi hiyo.

Aidha, unatakiwa kukiri kupokea "Offer" hii kwa maandishi ili Halmashauri ya Manispaa ya Lindi iweze kukupatia "Control number" kwa ajili ya kufanyia malipo hayo kwa mujibu wa sheria na taratibu za fedha.

Karibu uwekeze kwetu kwa maendeleo yako, yetu na Taifa kwa ujumla.

  
Jomaary Mwisho Satura  
Mkurugenzi wa Manispaa  
LINDI

**MKURUGENZI WA MANISPAA**  
**LINDI**

**Nakala:**

❖ Katibu Tawala wa Mkoa  
S.L.P 1054  
LINDI

- kwa taarifa

27/27

# AFRICAN CARIBBEAN SELF-HELP ORGANIZATION COMPANY LTD

P.O. Box 14190, Dar Es Salaam Tanzania  
Tel:+255 754 261341 Email: acshofarm@gmail.com

Kumb Na: ACSHO/LINDI 02/2019

8 Agosti, 2019

Mkurugenzi wa Manispaa,

Manispaa ya Lindi,

S. L. P 1070,

LINDI

## YAH: 'OFFER' YA EKARI 500 KWA AJILI YA KILIMO KATIKA ENEO LA JANGWANI

Tafadhali rejea barua yako ya tarehe 7 Agosti, 2019 yenye kumbukumbu namba LMC/D.10/6/31 kuhusu ombi letu la kupatiwa ekari 500 kwa ajili ya kilimo cha ufuta.

Tunakiri kuipokea barua hiyo na tunashukuru sana kwa kutukubalia ombi letu. Tukotayarikufanyamalipotukipewa 'control number' kamatutakavyoelekezwa. Tunaahidi kushirikiana na mamlaka husika kuhakikisha tunafanya kilimo kitaalamu kwa manufaa ya kampuni, jamiii inayo tuzunguka na taifa kwa ujumla.

Tunafurahi kuanza na ekari 500 wakati huu ambapo imetimia miaka 500 tangu mababu wawenzetu tunaoshirikiana nao kuwekeza pamoja walipo ondolewa bila hiari yao kutoka Bara mama la Afrika.

Asante sana.



Michael Carty

**MKURUGENZI**

AFRICAN CARIBBEAN SELF-HELP  
ORGANIZATION  
COMPANY LTD  
P.O. BOX 14190  
DAR ES SALAAM



Selvin Anderson

**MKURUGENZI WA FEDHA**

Nakala: KatibuTawala wa Mkoa,

S. L. P. 1054

LINDI